# UJUMBE MAALUM KUTOKA KWA HADHRAT MIRZA MASROOR AHMAD, KHALIFATUL MASIH V WA JUMUIYA YA WAISLAM WAAHMADIYYA KATIKA KUADHIMISHA KARNE YA UKHALIFA WA KIAHMADIYYA 1908 – 2008.

MIRZA MASROOR AHMAD
HEAD OF THE AHMADIYYA COMMUNITY

بسم الله الرحمن الرحيم
نحمده و نصلي على رسوله الكريم
وعلى عبده المسيح الموعود
خدا کے فضل اور رحم کے ساتھ
هو الناصر

**Wapendwa wangu Wanajumuiya wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya**
**Assalaam Alaikum warahmatullah wabarakaatuh**

**Hivi leo (tarehe 27 Mei 2008) imetimia karne moja ya Ukhalifa wa Kiahmadiyya. Siku ya leo inapeleka fikra zetu kwenye historia ya Jamaat Ahmadiyya ambayo imekuwepo kwa miaka mia moja, pia inatupeleka katika wakati ule wa bishara ya Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. ya kwamba mtumishi mteule wa Allah kwa amri yake, alitoa**

tangazo tarehe 23 Machi 1889 juu ya kuanzishwa kwa Jamaat takatifu. Dhamira ya kuanzishwa kwa Jamaat hii ilikuwa ni kuanzisha uhusiano baina ya Mwenyezi Mungu na binadamu, kumfundisha mwanadamu kujitupa kwa Mwenyezi Mungu Mmoja, kujitahidi kusimamisha tauhidi duniani na kuunganisha mataifa yote katika umma mmoja, kukusanya binadamu wote chini ya bendera ya Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. na kutanababahisha binadamu juu ya kutambua na kuheshimu haki za binadamu wote.

Mtu huyo ambaye Mwenyezi Mungu amemvisha cheo cha Imam, Masihi na Mahdi ameshakuja duniani na kwa mafanikio alitimiza wajibu wake kwa msaada wa Allah kwa takribana miaka kumi na tisa – yaani kuanzia mwaka 1889 hadi 1908 alipoaga dunia – licha ya upinzani wa kila aina na mazingira magumu, kila adui aliyemgusa huyu askari wa Allah alisagwa tikitiki na kuishia kwenye aibu na fadhaa.

Sawa na suna za Allah, kila ajaye duniani hatimaye lazima aondoke, na Mtumishi huyo mteule wa Allah na Mpenzi wa kweli wa Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w., dawamu kama ilivyokuwa sunna ya Bwana wake s.a.w. alikuwa na shauku ya kukutana na Rafiki yake Aliyetukuka. Allah Mwenye nguvu aliyemtuma mtumishi wake kuwa Imam

**Akhiruzzaman, wakati akimpa ishara kuwa siku za kuishi kwake zilikuwa zinakaribia kwisha, alimliwaza kwa kumhakikishia kuwa ingawaje kifo chake kilikuwa karibu lakini hataacha ujumbe wake usitimize malengo yake, kwani sawa na tamko lake Yeye ndiye aliyemuinua kuwa Imam wa siku za mwisho. Hivyo Mpendwa wangu: Ewe uliye na shauku ya kusimamisha Tauhidi Yangu duniani na Mamlaka ya Mtume wangu mpendwa usiwe na wasiwasi juu ya jinsi gani ujumbe wako utakavyotekelezwa pindi ukisha kufa. Kumbuka ya kuwa sawa na bishara ya Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. ambayo inaungwa mkono na mimi, Ukhalifa katika nyayo za utume utasimamishwa na utadumu hadi mwisho wa dunia. Hivyo ukisha ondoka ni taasisi hii hii ya Ukhalifa ambayo kwa kuitumia hii nitasimamisha sheria yangu ya mwisho duniani. Hivyo, baada ya kupata uhakikisho huo kutoka kwa Allah, Masihi Aliyeahidiwa aliiambia Jamaat:**

**“Hii ndiyo sunna ya Allah na tangu amuumbe binadamu duniani amekuwa akidhihirisha njia hii kwa kuwasaidia Mitume wake na kuwapa ushindi.**

**Anasema** كَتَبَ اللّٰهُ لَاَغْلِبَنَّ اَنَا وَرُسُلِيْ **maana yake Mwenyezi Mungu amekadiria kuwa Yeye na Mitume wake watashinda. Na kwa ushindi maana yake Mitume na watumishi wanahitaji Hujjat (matakwa yake) yasimamishwe duniani na kusiwe na yeyote anayeweza kudiriki kupinga matakwa hayo, hivyo Mwenyezi Mungu kwa alama zake zenye**

nguvu hudhihirisha ukweli Mitume wanaotaka kuueneza duniani na kuwapa fursa kupanda mbegu kwa mikono yao. Hata hivyo, matunda hayaivi wakati wapo, isipokuwa huwafisha wakati ambapo huonekana wameshindwa na hapo hutoa fursa maadui wacheke, wakebehi na kuwachezea shere Manabii. Na wanapokwisha kufanya yote hayo ya kebehi na kubeza, hapo ndipo hudhihirisha mkono wake wa pili wa nguvu na hutengeneza njia za kuyafikia yale malengo ambayo yalikuwa bado hayajafikiwa. Hivyo hudhihirisha nguvu za aina mbili.

1. Kwanza hudhidhirisha mkono wake wa nguvu kwa kupitia Mitume wenyewe.
2. Pili, wakati ambapo Nabii amekwishafariki, waaminio hukumbana na matatizo na adui hupata nguvu za kufikiri sasa kila kitu kimeangamia (kuhusu ujumbe wa Nabii) na kwamba wakati wa Jamati ya Nabii kuangamia na kutoweka kabisa kwenye uso wa ardhi umefika na hata waaminio hukata tamaa na kujiona watu wasiokuwa na matumaini na wale wenye bahati mbaya wanaamua kuritadi, hivyo Mwenyezi Mungu kwa mara ya pili anaonesha nguvu zake na hutoa msaada na hulinda Jamaat ambayo ilikuwa ukingoni mwa shimo tayari kuanguka. Hivyo mtu anayeendelea kuonesha msimamo thabiti hadi mwisho, huona miujiza ya

**Mwenyezi Mungu. Kama ilivyotokea wakati wa Hadhrat Abubakar Swiddiq ilipofikiriwa kwamba Mtume Mtukufu alikufa wakati usio muafaka, mabedui wengi wajinga wakaritadi. Masahaba wa Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w nao walishikwa na huzuni kubwa wakawa kama watu waliopoteza fahamu. Katika hali hiyo ya mashaka makubwa Allah akamuinua Abubakar Siddiq na akadhihirisha kwa mara ya pili mdhihiriko wa nguvu zake na Islam ambayo ilikuwa karibu kuanguka ilipewa msaada na Yeye na akatimiza ahadi yake iliyomo katika aya hii:**

وَ لَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِيْنَهُمُ الَّذِى ارْتَضٰى لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُمْ مِّنْ بَعْدِ خَوْفِهِمْ اَمْناً ط

**Yaani: Na Kwa yakini Atawaimarishia dini yao Aliyowapendelea, na Atawabadilishia amani baada ya hofu yao.** **(Risala Al-Wasiyyat, Ruhani Khzain Jal. 20, uk 304, 305)**

**Aliandika tena:**

**Basi, enyi wapenzi, kwa kuwa hii ndiyo sunna ya Allah tangu kale, ya kwamba Mwenyezi Mungu Huonyesha kudra mbili ili kufuta furaha mbili za bandia za wapinzani, hivyo haiwezekani sasa ya kuwa Mwenyezi Mungu Aiache sunna yake ya zamani. Kwa hiyo msihuzunike kwa habari niliyowaambieni wala nyoyo zenu zisifadhaike, kwani hamna**

**budi kuiona kudra ya pili vilevile. Na kuja kwake ni bora kwenu kwa sababu hiyo itadumu, nayo itaendelea bila kukoma mpaka Kiyama. Na hiyo kudra ya pili haiwezi kuja mpaka niondoke. Lakini niondokapo, hapo Mungu Atakutumieni hiyo kudra ya pili itakayodumu nanyi milele kama Mungu Alivyoahidi katika Barahini Ahmadiyya. Ahadi hiyo hainihusu mimi bali yawahusuni ninyi, kama Alivyosema kwamba Nitashindisha Jumuiya hii inayokufuata juu ya wengine hadi Kiyama. Basi hakuna budi mfikiwe na siku ya mimi kuagana nanyi ili baadaye iwadie ile siku iliyo siku ya ahadi ya kudumu. Mungu wetu huyu ndiye Mungu Atimizaye ahadi, Mwaminifu na Mkweli. Atawaonyesheni yote Aliyoahidi. Ijapokuwa hizi ni siku za mwisho za dunia na ndiyo zama za balaa nyingi kushuka, lakini hakuna budi dunia hii ibaki mpaka yote hayo yatimie Aliyoniambia Mungu. Mimi nimedhihirika nikiwa kudra moja kutoka kwa Mungu, nami ndimi kudra hasa ya Mungu na baada yangu watakuwapo wengine watakaokuwa onyesho la kudra ya pili. Hivyo basi, endeleeni kuomba mkiwa pamoja ili kuingoja kudra ya pili ya Mungu. Na yawapasa wanajumuiya wema wa kila nchi wakiwa pamoja kwamba wadumu kuomba.** (Risala Al-Wasiyyat, Ruhani Khzain Jal. 20, uk 305, 306)

**Hatimae, kama alivyosema Masihi Aliyeahidiwa a.s. wakati ulifika alipoaga dunia na**

**kwenda kwa Allah na moyo wa kila Ahmadiyya ulijaa hofu na wasiwasi. Hata hivyo, kwa sababu ya maombi ya waaminio mbingu na ardhi zilishuhudia kutimia kwa ahadi:**

**وَلَيُبَدِّلَنَّهُمْ مِّنْ بَعْدِ خَوْفِهِمْ اَمْناً ط na Atawabadilishia amani baada ya hofu yao. (24:56.)**

**Kama ilivyoshuhudiwa siku zilizopita. Mapinduzi makubwa ambayo aliyaleta kufuatia kudhihiri kwake yalikadiriwa na Allah yaendelee na kuimarika kupitia mfumo wa Ukhalifa.**

**Alipofariki Masihi Aliyeahidiwa a.s. Maulana Abdul Kalam Azadi (ambaye si Ahmadiyya) aliandika katika gazeti liitwalo Wakil:**

**“Huyo bwana, mtu maarufu ambaye kalamu yake ilikuwa ni muujiza mtupu na hotuba zake zenye mvuto wa ajabu, mtu aliyekuwa na maajabu ya ubongo ambaye kukutizama kwake kuliweza kukuteka na ambaye sauti yake ilikuwa ni wito kwenye ufufuo, ambaye vidole vyake vilikuwa vimeshika nyaya za mapinduzi na ambaye mikono yake ilibeba betri zilizo tayari za umeme, bwana huyu ambaye kwa miaka thelathini alisababisha matetemeko na dhoruba katika ulimwengu wa dini, ambaye alikuwa kama mpiga baragumu la siku ya miwsho, akaandelea kuwaamsha wale waliozama katika mambo ya dunia. Kifo cha Mirza Ghulam Ahmad Sahib wa Qadian ni kifo ambacho**

**mtu hawezi kukosa somo na kuacha tu kifo hicho kitiririke katika mkondo wa historia na ukajiridhisha. Watu wanaoleta mapinduzi katika ulimwengu wa kiroho na kisomi hutokea kwa nadra, watoto hawa maarufu wa historia, fahari ya binadamu hawafiki mara kwa mara na pindi watokeapo hawaondoki duniani hadi wameleta mapinduzi."**

**(Wakil, Amristar, (Tarik-e-Ahmadiyyat, Jal. 2, uk. 560).**

**Hivyo, kwa Mwenyezi Mungu kuwafanya wasio Waahmadiyya kukiri juu ya mapinduzi haya kwa ndimi zao na kalamu zao kunaonesha kuwa Masihi Aliyeahidiwa alikuwa na masaada maalum wa Allah. Lakini masikini hawakutambua kwamba Muumba mwenye uwezo mkubwa wa kuonesha maajabu, ndiye huyo huyo mwenye uwezo Aliyekuwa ameahidi kuwa kupitia kwenye neema za Ukhalifa ataendeleza mapinduzi yaliyoanzishwa na yule aliyekuwa ameungwa mkono na kusaidiwa na Allah na dunia yote ilishuhudia ukweli huo wakati wa uchaguzi wa Khalifa, wakati Hadhrat Maulana Nuruddin r.a. alipochaguliwa kuwa Khalifatul Masih I. Licha ya kwamba maadui wa Masihi Aliyeahidiwa kuona Jamaat yenye uongozi mzuri na iliyoungana iliyoanzishwa na Masihi Aliyeahidiwa (a.s.) na licha ya kuona tukio la kuanzishwa ukhalifa, walijitahidi kwa nguvu zote kuingamiza Jamati – Jamati ambayo ilianzishwa na Mwenyezi Mungu**

**mwenyewe na ambaye aliahidi: اُذْكُرْ نِعْمَتِیْ غَرَسْتُ لَکَ بِیَدِی رَحْمَتِی وَقُدْرَتِی**

**Kumbuka fadhila zangu, nimekupandia wewe mti wangu wa huruma na uwezo wangu kwa mkono wangu mwenywe (Tadhkira – 428).**
**Hivyo, kufuatana na ahadi hiyo wale maadui walishindwa vibaya kama ilivyo ada ingawaje walikwenda mbali katika upinzani wao hadi gazeti moja likaandika:**

**Mtu yeyote akituuliza, tuko tayari kusema kwa uhakika ya kuwa haja yetu hasa ni kwamba Waislamu wote ikiwezekana watupe vitabu vya Mirza sio baharini, lakini katika tanuru la moto, na wasiishie hapa isipokuwa waende mbele zaidi na wahakikishe ya kwamba wanahistoria wa baadae wawe ni Waislamu au wasio Waislamu hawataji jina lake katika historia ya India na Islam (Wakil, Amritsar, Juni, 3, 1908, Tarik-e-Ahmadiyya, Jal. 3, uk. 205, 206).**

**Lakini hivi leo, historia inadhihirisha kuwa Ahmadiyya inafahamika pembe zote za dunia na kwamba hakuna anayewakumbuka wapinzani wa Jamati.**
**Kwa hakika kupitia baraka za Ukhalifa, Ahmadiyya inashamiri na kunawiri duniani na mamilioni ya watu ni wafuasi shupavu wa Ahmadiyya au kwa maneno mengine Islam hasa.**

**Maadui wa Ahmadiyya walifikia kilele cha maneno yao ya kipuuzi wakati gazeti moja liitwalo Curzon Gazette, lilipoandika maneno haya yaliyorejewa na Hadhrat Khalifatul Masih I katika hotuba yake wakati wa Jalsa Salana:**
**"Sasa hakuna kilichobaki kwa hawa Mirzai, kichwa chao kimekatwa. Mtu mmoja aliyechaguliwa kuwa Imamu hana uwezo wa kufanya chochote isipokuwa kuwafundisha ninyi Waahmadiyya Qur'ani Msikitini"** (Tarikh-e-Ahmadiyya. Jal. 3, uk.221).

**Akizungumzia juu ya maneno hayo Khalifatul Masih I alisema: (Subhanallah – utukufu ni wa Mwenyezi Mungu), hili ndilo jukumu muhimu kabisa lenye kipaumbele kuliko kitu chochote . Namuomba Allah anipe wasaa kuendeleza jukumu hilo.**

**Kwa bahati mbaya baadhi ya Wanajumuiya mashuhuri, hawakutambua uzito (wa Ukhalifa) na mara nyingi Jamaat ilipambana na misukosuko na mateso hata hivyo kutokana na baraka za Ukhalifa, Jamaat ilivuka shwari katika mawimbi hayo na kupiga hatua mbele. Tukitazama kwa uangalifu miaka hamsini ya Ukhalifa wa Hadhrat Khalifatul Masih r.a. II tutaona ni kiasi gani alivyofaulu mwana huyu wa Mshindi wa Allah Masihi Aliyeahidiwa.**

**Baada ya kifo cha Hadhrat Musleeh Mauud (r.a) kwa mara nyingine ulimwengu wa Kiahmadiyya ulikumbwa na hofu, lakini Mwenyezi Mungu sawa na ahadi yake ya kuondoa hofu na kuleta utulivu, katika saa chache aliipatia Jamaat mwezi mpevu wa dhihirisho la tatu la Qudrat Thaaniya (Ukhalifa) licha ya upinzani wa serikali ya wakati huo na licha ya juhudi za pamoja za madhehebu ya kiislamu (kabla na baada ya kupitisha sheria zao za kikatili dhidi ya Ahmadiyya), msafara wa Ahmadiyya ulizidi kusonga mbele, huku ukipata maendeleo makubwa na kuipa dunia ujumbe wa mapenzi, kuwatumikia masikini, katika nchi masikini na kuwafikishia ujumbe wa Nabii kutoka Uarabuni na kuwaweka chini ya bendera yake.**

**Halafu wakati ukaja sawa na uamuzi wa kimbinguni, Hadhrat Khalifatul Masih III aliondoka katika dunia hii ili kukutana na Muumba wake. Kwa mara nyingine matatizo ndani na nje yakajitokeza. Lakini sawa na ahadi ya Mwenyezi Mungu, Jamaat Ahmadiyya ilijidhatiti na kuimarika kupitia kwa Khalifatul Masih Rabii na kila hila zikatokomea.**

**Allah, mwenye uwezo akawaangamiza wale walioweka vikwazo kwenye Jamaat kwa kupitia sheria za kikatili na wale waliojigamba kwamba wangeweza kuangamiza kile**

walichokiita "Saratani ya Ahmadiyya". Kwa sababu ya sheria hii iliyopitishwa na serikali ya Pakistani Khalifa wa wakati huo ilibidi kuhama, lakini hijira hii ikafungua milango kwa ajili ya maendeleo ya Ahmadiyya. Kwa mara nyingine tukaona kutimia kwa ahadi: غَرَسْتُ لَکَ بِیَدِی

Milango mingine mingi ya ubashiri iliyokuwa imefungwa ikafunguliwa wakati wa Khalifa wa nne, Mwenyezi Mungu kwa kupitia **MTA** akatimiza ahadi yake kwa Masihi Aliyeahidiwa (a.s) kuwa: میں تیری تبلیغ کو زمین کے کناروں تک پہنچاؤں گا
"Nitafikisha ujumbe wake kwenye pembe zote za dunia." Jambo hili ni la ajabu ukitizama hali yetu ya mapato na jinsi kituo hiki kilivyoanza, ni dhahiri maneno ya Tasbih (kumtukuza Allah) na Tahmid (kusifu) yatabubujika kutoka kwenye ndimi za waaminio. Hivi leo, kituo hiki, kutoka mashariki hadi magharibi, kutoka kaskazini hadi kusini kimewanyamazisha maadui wa Ahmadiyya. Hivyo Mwenyezi Mungu Ameteremsha kupitia **MTA** sauti ya mtu anayeeneza ujumbe wa ukweli katika nyumba za wale waliotaka kumnyamazisha Khalifa wa wakati huo, hivi leo kupitia MTA chakula cha kiroho (Maida) cha ulim - e - kalam chini yake na hoja zake zinazolinda ukweli wa Islam na kwa ajili ya kujibu hoja na misingi ya imani nyingine na kueneza sheria

ya mwisho ya Mwenyezi Mungu - Qur'an Tukufu ambayo kwa msaada wa Mwenyezi Mungu imefika kila nyumba sawa na kanuni/sheria iliyotajwa katika aya: كُلُّ مَنْ عَلَيْهَا فَانٍ "Kila kilichomo juu yake kitatoweka .... " (55:27), Khalifatul Masihi IV alifariki. Na wakati huo wa kifo chake dunia nzima kupitia jicho la MTA iliweza kuona tukio hili. Tukio hili lilikuwa la kufurahisha kwani Waahmadiyya na wasio Waahmadiyya walifurahi ya kwamba Mwenyezi Mungu baada ya hofu yao Amewapa utulivu na wengine wakaendelea kushangaa jinsi gani Jumuiyya hii waliyokuwa wanajaribu kuangamiza katika miaka mia ilivyokuwa inazidi kusitawi na kuendelea. Mpinzani mmoja alikubali wazi wazi "Siamini kwamba ninyi mko katika njia iliyonyooka lakini baada ya kuona hili lazima nikiri kwamba Mwenyezi Mungu kwa tendo hili Amedhihirisha kuwa yu pamoja nanyi."

Mimi ni mtu dhaifu na sina elimu kubwa lakini Allah Mwenye uwezo Ameunganisha chini ya mkono wangu Jamaat nzima, kila siku uhusiano baina yangu na Jamaat unakuwa kwa mapana na marefu. Dunia ilifikiri labda nitashindwa kuiongoza Jamaat na kwamba wataona mwisho wa Jamaat, jambo ambalo wamekuwa wakilisubiri kipindi cha miaka mia moja. Lakini wakasahau kwamba mti huu umepandwa na Mwenyezi

**Mungu, hakuna mwanadamu anayehusika na mpango au kusitawi kwa mti huu. Kwa hakika, chochote kinachotokea kinatokea kwa sababu ya ahadi ya Mwenyezi Mungu na msaada wake, na Mwenyezi Mungu Anatimiza Ahadi Aliyompa Masihi Aliyeahidiwa katika ufunuo; "Niko pamoja nawe na wale unaowapenda"**

**Hivyo ni uamuzi wa kimbinguni. Hii ni ahadi ya Mungu Yule Asiyetoa ahadi za uongo - ahadi ya kwamba wale wapendwa wa Masihi Aliyeahidiwa ambao kufatana na mafunzo yake, wamepokea dhihirisho la pili la uwezo wa Allah na ndio watakaoiongoza dunia, kwani Mwenyezi Mungu yu pamoja nao, Mwenyezi Mungu yu pamoja nasi. Hivi leo miaka 100 ya dhihirisho la pili la Nguvu za Allah imetimia, na kila siku tunashuhudia kutimia kwa ahadi hiyo iliyotajwa na Mwenyezi Mungu kwa Masihi Aliyeahidiwa na kama shani inavyozidi kudhihirika kama tulivyoeleza katika historia fupi ya Jamaat tuliyotoa. Hivyo ni wajibu wa kila Ahmadiyya wakati anaendelea kuunganika na dhihirisho la pili la Allah ajitahidi kwa nguvu zake zote kutekeleza ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa (a.s).**

**Hivi leo tunawajibika kuwaleta Wakristo wote chini ya bendera ya Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w), tunawajibika kuwaleta pia Mayahudi chini ya bendera, na**

tunalazimika kuwaleta Wahindu wote na wafuasi wa dini nyingine chini ya bendera ya Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w).

Pia tunawajibika kuwaunganisha Waislam wote duniani ili wajiunge na Khilafat - e - Ahmadiyya kwa Mkono wa Masihi Aliyeahidiwa (a.s)

Waahmadiyya mnaoishi pembe zote za dunia popote mlipo zingatieni sana jukumu hili la msingi nililowaelezeni na kazi ambayo Imam - uz - zamani, Masihi Aliyeahidiwa amewapa kwa amri ya Allah. Masihi Aliyeahidiwa kwa kusema kwamba; "ahadi hii ni kwa ajili yenu" ametutwisha wajibu mkubwa. Na ahadi zinatimizwa tu wakati Masharti yanayoambatana na ahadi hizo yanatekelezwa.

Waaminio wa Masihi - e - Muhammad (Masihi wa Muhammad), wapendwa wa Masihi Aliyeahidiwa na matawi mawili ya mti wake, simameni kuweni tayari kutoa zabihu ya aina yoyote inayotakiwa ili kuinurisha **Khilafat - e - Ahmadiyya** na kwa kushika kwa nguvu kamba ya Allah, muweze kueneza duniani kote, ujumbe wa Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w), kiongozi na Muta (anayetiiwa) wa Masihi Aliyeahidiwa,

ujumbe ambao Mwenyezi Mungu alimpa Masihi Aliyeahidiwa aueneze. Pia fikisheni ujumbe kwa kila binadamu mkiwaeleza kuwa uhai unategemea kuanzisha kuwa na mahusiano na Mungu mmoja na kwamba amani ya dunia inategemea kujiunga na Jamaat ya Mahdi na Masihi kwani hivi leo yeye pekee ndiye aliyesimamisha bendera hasa ya Islam inayoonyesha mafundisho halisi juu ya amani na ulinzi, na mafunzo hayo hayana mfano wako katika uso huu wa ardhi. Hivi leo, kutekeleza ujumbe wa Masihi wa Muhammad (s.a.w) na kuunganika kiimani katika umoja wa Mwenyezi Mungu, hayo yote yanawezekana tu kwa kuendelea kufungamana na Khilafat - e - Ahmadiyya. Ni kwa njia hii watu wa Mungu wataleta mapinduzi ya kiroho duniani.

Mwenyezi Mungu Amuwezeshe kila Ahmadiyya kufikisha kwa kila mtu ukweli huu wa thamani.

Wassalaam

Khaksar

**(Mirza Masroor Ahmad)**

**(Khalifatul Masih V)**